**BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA TATU**

**Kikao cha Kumi na Nane – Tarehe 28 Mei, 2021.**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

## I. MASWALI:

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

74. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa,Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Katika kukabiliana na matatizo mbali mbali katika skuli za maandalizi na msingi, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, imeanzisha utaratibu wa kuzipatia skuli hizo fedha kwa ajili ya uji wa wanafunzi pamoja na gharama za umeme na maji. Hatua hiyo iliwasaidia sana wanafunzi hasa wale wanaoishi katika mazingira magumu. Hata hivyo, kuanzia mwezi Agosti, 2020 hadi sasa, utoaji wa fedha hizo kwa skuli nyingi umekuwa wa kusuasua na kuleta shida kwa viongozi wa skuli hizo.

(a) Je, Serikali inalitambua tatizo hili na kama inalitambua, imejipangaje kukabiliana nalo.

(b) Ni kiasi gani cha fedha kinachotolewa kwa skuli ya Manispaa ya Magharibi “A” kwa kila mwezi.

**Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:**

182. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Katika lengo la Bajeti la mwaka 2020/2021, Serikali ilikusudia kuimarisha Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa kutoa mikopo yenye thamani ya shilingi milioni kumi.

(a) Je, lengo hili limefikiwa katika hatua gani.

(b) Je, ni wananchi wangapi waliopata mikopo hiyo.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

2. MHESHIMIWA SHAABAN ALI OTHMAN (Jimbo la Mpendae) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Vituo vingi vya kuuzia mafuta (hasa Petrol) vimekuwa vikijengwa karibu na makaazi ya wananchi, jambo ambalo linahatarisha usalama wa wananchi na makaazi yao, iwapo itatokezea janga la moto.

Kwa kuzingatia athari za kiafya na kimazingira zinazoweza kuwapata wananchi wa Zanzibar wanaoishi karibu na vituo hivyo.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kukabiliana na kunusuru hali hiyo.

(b) Kwa vile Mamlaka husika za kudhibiti hali hiyo zipo na hali ya ujenzi wa aina hiyo bado unaendelea kote nchini. Je, Serikali inachukua hatua gani kwa watendaji wa Taasisi hizo.

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

20. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani)

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Katika suala la kupunguza umasikini pamoja na kujiongezea mapato, akina mama wengi katika maeneo ya Kojani na vijiji vyake wameamua kuwekeza katika ushonaji au usukaji wa mikoba ya ukili, vikapu, mikeka na

usukaji wa aina tofauti. Kwa kuwa akina mama hawa hutegemea zaidi soko la ndani “local market” ambalo halina dhamana.

(a) Je, ni lini Serikali itawajengea uwezo akina mama wa vijiji vya Kojani, Chwale, Likoni na Mchanga mdogo.

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia soko la uhakika la ndani na nje ya nchi.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

161. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kwa kuwa Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba kwa wakati ule ambaye sasa ni Makamu wa Pili wa Rais aliomba kumaliziwa kwa kipande kilichobakia hadi kufikia Mtambile ili kuifanya barabara hiyo iwe ni kiunganishi muhimu na barabara kuu iliyotoka Chake Chake hadi Mkoani.

(a) Je, hatua za ujenzi wa kipande hicho zimefikia wapi

(b) Je, ni lini wananchi wa kisiwa cha Pemba watarajie kukamilika kwa barabara hiyo.

**Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:**

54. MHESHIMIWA YAHYA RASHID ABDULLA (Jimbo la Kwahani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

Gharama za kupima maradhi ya Covid 19 kwa Wazanzibari wanaosafiri kwenda nje ya nchi zimepanda sana hadi kufikia shilingi 185,000/- za kitanzania.

(a) Je, ni sababu gani zilizopelekea gharama hizo kupanda.

(b) Je, Serikali haioni umuhimu wa kupunguza gharama hizo kwa wanafunzi wanaosoma nje ya nchi ili kuwapunguzia gharama hasa ikizingatiwa kuwa pia hulipa tena wanapofika nchi wanazosoma.

**<u>Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:</u>**

186. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Katika shabaha ya mwaka 2020/2021 ya Wizara ya Kilimo ni kuendeleza kufuatilia uzalishaji wa mazao ya viungo katika eneo la hekta kumi (10) za mashamba ya mipira Unguja na Pemba kwa ajili ya usafirishaji nje ya nchi ikiwemo vanila, pilipili hoho, manjano, tangawizi na pilipili manga.

(a) Je, ni hatua gani iliyofikiwa katika kilimo hicho.

(b) Je, ni hekta ngapi mpaka sasa zilizolimwa zao la pilipili hoho.

## II. <u>HOJA ZA SERIKALI:</u>

**<u>Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:</u>**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto kwa mwaka 2021/2022.

**Zanzibar,**
**28 Mei, 2021.**

**(Raya Issa Msellem)**
**<u>KATIBU WA BARAZA</u>**